

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
WAKALA WA VYUO VYA MAFUNZO YA MIFUGO



CHAKULA BORA CHA MIFUGO



Kimetayarishwa na:

Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA)
Kampasi ya Morogoro
S.L.P. 603,
MOROGORO – TANZANIA
E-mail: litamorocamp@gmail.com

UTANGULIZI

Chakula bora ni msingi mkubwa katika uzalishaji kwenye sekta ya mifugo, ili kupata chakula bora cha mifugo lazima mfugaji azingatie

- Upatikanaji wa malighafi
- Gharama za malighafi
- Ubora wa malighafi
- Mahitaji ya mnyama husika
- Usafi wa Mazingira husika
- Mipaka ya matumizi ya malighafi
- Utunzaji wa chakula baada ya kutengeneza

Malighafi

Zipo aina mbalimbali za malighafi zinazotumika kutengeneza chakula cha mifugo ikiwemo

- Mashudu ya pamba
- Mashudu ya alizeti
- Mahindi paraza
- Damu lilyosagwa
- Pumba za mahindi
- Chenga za mchele
- Maharagwe (soybean)
- Dagua/sangara
- Mifupa
- Chokaa
- Mineral and vitamin Premixes
- Chumvi
- Methionine

Aina za malighafi zinategemeana na mahali ulipo, tumia malighafi ambayo inapatikana mahali ulipo ila zingatia hitaji la mnyama kulingana na umri wa mnyama, uzalishaji wake, jinsia yake na ina ya mnyama pamoja.

Aina ya vyakula

Kuna aina mbalimbali ya vyakula kutegemea na hitaji la mnyama kama ifuatavyo:

Kuku wa nyama wadogo wiki (0-4) aina hii ya kuku wanahitaji kiwango kikubwa cha protein kisichopungua 20-23%CP kwenye mlo wao kwasababu wanahitaji kukua

Kuku wa nyama wakubwa wiki (4-8)

Kuku hawa wanahitaji kiwango kikubwa cha nguvu kisichopungua 13-15MJ nakiwango cha protein 18-20%CP kwenye mlo wao.

Kuku wa kienyeji

Kuku hawa wanahitaji kiwango cha protein kisichopungua 15-18% CP na kiwango cha nguvu 11-15MJ kwenye mlo wao hasa wale wafugwao ndani

kuku wa mayai wiki (0-8)

Kuku hawa wanahitaji kiwango kikubwa cha protein kisichopungua 21-23%CP na kiwango cha nguvu 13-15MJ.

Kuku wa mayai wanaokuwa wiki (9-18)

Kuku hawa wanahitaji kiwango cha protein kisichopungua 14-16%CP na kiwango cha nguvu 11-13MJ.

Kuku wanaotaga

Kuku hawa wanahitaji kiwango cha protein kisichopungua 15-17%CP na kiwango cha nguvu 13-15MJ kwenye mlo wao pamoja na kalshium(3-4) %

Ngombe wa maziwa

wanahitaji kiwango cha protein kisichopungua 14-16%CP pamoja na calcium 0.5-0.6%

Nguruwe wadogo

wanahitaji kiwango kikubwa cha protein kisichopungua 17-18%CP.

Nguruwe wakubwa

Wanyama hawa wanahitaji kiwango cha protein kisichopungua 15%CP na kiwango cha nguvu 13-15MJ kwenye mlo wao

Madhara ya ukosefu wa chakula bora Kwa Ujumla

- Kupunguwa kwa kiwango cha uzalishaji
- Kuku kuchelewa kutaga
- Kuchelewa kukua
- Kushidwa kuingia kwenye joto kwa wakati
- Kudumaa
- Magojwa hasa yanayotokana na lische duni kama;
 - a. Matega
 - b. Kichaa cha vifaranga
 - c. Homa ya maziwa
 - d. Kuwa na ngozi kavu

Zingatia

Hakikisha unafika LITA (Livestock Training Agency) upate ujuzi ili inufaike na ufugaji bora kwa uchumi wa viwanda na maendeleo ya Taifa.